ISSN 1866-5866 APRILI - JUNI 2025

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
TANZANIA COMMISSION FOR HUMAN RIGHTS AND GOOD GOVERNANCE

# THE VOICE OF Haki

JARIDA LA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

# WANANCHI WAENDELEA KUITUMIA THBUB KUWASILISHA MALALAMIKO



*Makamu Mwenyekiti Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora(THBUB) Mhe.Mohamed Khamis Hamad, (katikati) katika picha ya pamoja na Makamishna wengine wa THBUB Mhe.Dkt.Thomas Masanja, (wa Pili kushoto, Mhe.Khatib Mwinyi Mwinyichande (wa Tatu kushoto), Mhe.Amina Talib Ali (wa pili kulia) na Mhe.Nyanda Shuli (wa kwanza kulia) wakiwa katika picha ya Pamoja na baadhi ya Menejimenti wa THBUB Pamoja na Wadau kutoka Asasi za kiraia, katika kikao cha kupitia maoni ya wasau katika kutekelezaji wa Itifaki ya Maputo Julai 2,2025 katika Hoteli ya Golden Tulip Dar es Salaam.*

NDANI THBUB YAIMARISHA HAKI YA KUISHI KWA KUPANDA MITI

# NENO LA UTANGULIZI

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ni idara huru ya Serikali, iliyoanzishwa kama Taasisi ya kitaifa iliyo kitovu cha kukuza na kulinda Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora nchini Tanzania.

THBUB ilianzishwa chini ya Ibara ya 129(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 3 ya mwaka 2000.

THBUB imepewa jukumu la kupokea na kuchunguza malalamiko ya uvunjifu wa haki za binadamu, kufanya ufafiti,ufuatiliaji wa masuala ya haki za binadamu na utawala bora sambamba na kutoa elimu.



**Mhe. Mathew Mwaimu (Jaji mstaafu)**
**Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Uanzishwaji wa jarida la Voice of Haki umelenga kuonesha kazi mbalimbali zinazofanywa na THBUB ili kuweka uelewa kwa jamii kuhusu majukumu ya Tume na namna majukumu hayo yanavyotekelezwa katika kulinda na kukuza haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Hivyo, nichukue fursa hii kuwakaribisha kusoma jarida hili kuweza kuifahamu THBUB Pamoja na majukumu yake.

**KAMATI YA UHARIRI**
Mwenyekiti:
Monica Mnanka
**Mhariri**:
Zawadi A. Msalla
Mhariri Msaidizi:
Nuru Mfaume
**Wajumbe:**
Mwashamba Juma
Tumaini Obel
Farida Ruben

**MAWASILIANO**
Mtaa wa Nyerere,
Plot Na. 339/Kilimani
S.L.P 1049 DODOMA,
Tanzania
Simu: +255 738 279744
Barua Pepe:
www.chragg.go.tz

## YALIYOMO

| | |
|---|---|
| THBUB YASAJILI MALALAMIKO MAPYA 160 | UK. 4 |
| WATUMISHI THBUB WATAKIWA KUTOA HUDUMA BORA KWA WANANCHI | UK. 5 |
| THBUB YAITAKA SERIKALI NA WAAJIRI NCHINI KUENDELEA KUWEKA MAZINGIRA BORA YA KAZI | UK. 6 |
| THBUB YALAANI VIKALI VITENDO VYA UKIUKWAJI WA HAKI ZA BINADAMU NCHINI | UK. 7 |
| THBUB YATOA RAI KWA WANANCHI WA KATA YA ILEMBULA MKOANI NJOMBE KULINDA HAKI ZA BINADAMU. | UK. 8 |
| WATUMISHI WA THBUB WATAKIWA KUZINGATIA MAADILI YA UTUMISHI WA UMMA | UK. 9 |
| VIJANA WAASWA KULINDA AMANI NCHINI | UK. 10 |
| THBUB NA DIHR ZAWAJENGEA UWEZO WATUMISHI KUHUSU HAKI ZA WAVUVI WADOGO | UK. 11 |
| THBUB YATOA ELIMU YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA KWA MAAFISA WA JESHI LA POLISI | UK. 12 |
| THBUB YAHIMIZA WANANCHI KUPATA USHAURI WA KITAALAMU ILI KUJUA SHERIA ZA ARDHI. | UK. 13 |




***Afisa Uchunguzi Mkuu kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Bi. Juliana Laurent akitoa huduma kwa mwananchi aliyefika katika banda la THBUB kwenye kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia viwanja vya Maturubai Mbagala, Jijini Dar es salaam Juni 16, 2025.***




***Baadhi ya Waandishi waendesha Ofisi, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa kikao kazi cha Taaluma hiyo kilichofanyika Jijini Arusha Mei 12 hadi 17, 2025.***

# Wananchi waendelea kuitumia THBUB kuwasilsha malalamiko

Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Hayo aliyasema Waziri wa Katiba na Sheria, Dkt. Damas Ndumbaro wakati alipokuwa akiwasilisha Bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/26.

Alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, THBUB ilianza na malalamiko 759 na kusajili malalamiko mapya 160 kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 hivyo kufanya jumla ya malalamiko hayo kuwa 919.

Pamoja na taarifa ya usajii wa malalamiko, aliainisha kazi zitakazotekelezwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika Mwaka wa fedha 2025/2026 kuwa ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika mikoa 26 ya Tanzania bara na mikoa mitano ya Zanzibar. Kazi nyingine ni kushughulikia malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na kufanya ufuatiliaji wa mapendekezo ya THBUB 104 yaliyo wasilishwa kwenye taasisi za umma na binafsi; kufanya ukaguzi wa maeneo walimozuiliwa watu kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Magereza, Vituo vya Polisi, Mahabusu za Watoto na vyuo vya mafunzo) na kufanya ufuatiliaji, utafiti na tathimini ya hali ya haki za binadamu na utawala bora nchini



*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe.Dkt. Damas Ndumbaro akiwasilisha bungeni utekelezaji wa majukumu , mapato na matumizi  ya THBUB kwa mwaka wa fedha 2025/26 Jijini Dodoma Aprili30,2025*



***Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt. Franklin Jasson Rwezimula akizungumza na baadhi ya Watumishi wakati alipotembelea Banda la THBUB katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Viwanja vya Chinangali Dodoma Juni 23, 2025***

# WATUMISHI THBUB WATAKIWA KUTOA HUDUMA BORA KWA WANANCHI

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt Franklin Jasson Rwezimula ametoa wito kwa Watumishi wa Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi ili kuwawezesha wananchi hao kupata haki zao.

Dkt Rwezimula ametoa wito huo Juni 23, 2023 wakati alipotembelea Banda la THBUB wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma.

Dkt. Rwezimula amesema kuwa wananchi wanapopata changamoto ya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora wanaamini kuwa THBUB ndipo mahala sahihi pa kupata haki zao

“…..Hivyo, nanyi mshughulikie malalamiko yao kwa ueledi na ufanisi ili wapate haki zao… .”amesema Dkt. Rwezimula Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yalifunguliwa Juni 16,2025 ikiwa na lengo kuwahudumia Watumishi wa Umma na Wananchi kwa pamoja na yalikuwa na kaulimbiu

***“Himiza matumizi ya mfumo wa Kidijitali ili kuongeza upatikanaji wa taarifa na kuchagiza uwajibikaji.”***

# SERIKALI NA WAAJIRI NCHINI KUENDELEA KUWEKA MAZINGIRA BORA YA KAZI

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeitaka Serikali na waajiri wote nchini kuendelea kuweka mazingira bora ya kazi na kusimamia maslahi ya wafanyakazi kwa mujibu wa katiba na sheria za ajira ili kujenga mazingira rafiki kwa wafanyakazi kufurahia haki zao za kufanya kazi.

Rai hiyo imetolewa na Mhe. Mathew Mwaimu (Jaji Mstaafu), Mwenyekiti wa THBUB alipokuwa akizungumza na Vyombo vya habari katika kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Aprili 30, 2025 Jijini Dodoma.

Mhe. Mwaimu amesema kuwa maadhimisho hayo yanalenga kutambua mchango wa wafanyakazi duniani kote katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

"Nitoe rai kwa Serikali na waajiri wote nchini kuendelea kuweka mazingira bora ya kazi na kusimamia vyema maslahi ya wafanya kazi kwa mujibu wa katiba na sheria za ajira ili kujenga mazingira rafiki kwa wafanyakazi kufurahia haki yao ya kufanya kazi na pia kuleta tija na ufanisi katika utendaji, amesema Mhe. Mwaimu (Jaji Mstaafu). Maadhimisho haya ya Mei Mosi mwaka 2025 yalienda sambamba na kaulimbiu isemayo ***"Uchaguzi Mkuu 2025 Utuletee Viongozi Wanaojali Haki na Maslahi ya Wafanyakazi, Sote Tushiriki Uchaguzi"***

Mhe. Mwaimu amesisitiza kuwa kauli mbiu hiyo inawahamasisha wafanyakazi kujitokeza kushiriki uchaguzi huo ili kuhakikisha kwamba pamoja na wananchi wengine wanashiriki kikamilifu kuwachagua viongozi wenye kusimamia na kulinda haki za binadamu.

Aidha, Mhe. Mwaimu amesema THBUB inatambua na kupongeza juhudi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha nchi inapata viongozi waadilifu, wasiyo na ubaguzi, wenye uzalendo, wanaoheshimu haki za Binadamu na kuzingatia misingi ya utawala bora katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuendelea kujenga taifa lenye amani na utulivu.

***Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Mhe.Mathew Mwaimu(JajiMst) akizungumza na waandishi wa Habari wakati akitoa tamko la Maadhimisho siku ya Wafanyakazi Duniani Aprili 30,2025***





*Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Mhe Mathew Mwaimu(JajiMst) akizungumza na Waandishi wa Habari wakati akitoa tamko kuhusu kupinga vitendo vya kikatili na ukiukwaji wa haki za binadamu nchini,Makao Makuu ya THBUB Jijini Dodoma Mei 5,2025*

# THBUB yalaani vikali vitendo vya ukiukwaji wa Haki za Binadamu nchini

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora nchini (THBUB) imelaani matukio mbalimbali yenye viashiria vya uvunjifu wa haki za binadamu nchini. Matukio hayo ni pamoja na lugha chafu zisizozingatia utu na heshima ya mtu, yanayoleta hamasa na kuchochea uvunjivu wa amani na utulivu, kushambuliwa na kujeruhiwa kwa baadhi ya wananchi na matukio yanayoashiria matumizi ya nguvu kupita kiasi wakati wa mikusanyiko ya kisiasa.

Hayo amesema Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora , Mhe. Jaji (Mst) Mathew Mwaimu wakati akizungumza na vyombo vya habari Jijini Dodoma Mei 05, 2025.

"Katika kipindi cha takriban mwezi mmoja na nusu, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imekuwa ikifuatilia kwa karibu matukio mbali mbali ambayo yamekuwa yakijitokeza nchini. THBUB baada ya kufanya tathmini kuhusu matukio hayo kwa mujibu wa katiba na sheria ya THBUB, imejiridhisha kuwa matukio hayo yanaashiria uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora."amesema

Akitolea mfano wa matukio hayo, Mhe. Jaji (Mst)Mwaimu ameelezea kusikitishwa na matukio ya kupigwa kwa Padri Dkt.Charles Kitima ambaye ni Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) na kutekwa kwa Faluka Saidi Nyagali (Mdude), Mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Pia, ameongeza kuwa THBUB inaona kuwa matendo yaliyojitokeza hayatoi taswira nzuri katika ustawi wa haki za binadamu, utawala bora na amani na utulivu hasa katika kipindi hiki kuelekea uchaguzi Mkuu.

Sanjari na hayo, Mhe. Jaji (Mst) Mwaimu amelitaka Jeshi la Polisi liendelee kuwasaka na kuwachukulia hatua za kisheria waliohusika na kujeruhiwa kwa Dkt. Charles Kitima, waliomteka Faluka Saidi Nyagali (Mdude) na waliohusika katika matukio mengine ya uvunjwaji wa haki za binadamu.

THBUB inatambua kuwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi, sheria za nchi na mikataba mbalimbali ya kimataifa ya haki za binadamu ambayo Tanzania imeridhia, wananchi wote wanayo haki ya kufurahia na kupata haki zao za binadamu.

"Kwa mujibu wa Katiba ya Nchi, kila mwananchi anayo haki ya kuishi, kuwa huru, kutoa maoni na kushiriki katika shughuli za umma moja kwa moja au kupitia wawakilishi kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa katika katiba na sheria za nchi," ameongeza Mhe. Jaji (Mst) Mwaimu.

# THBUB yatoa rai kwa wananchi wa kata ya Ilembula mkoani Njombe kulinda Haki za Binadamu.

Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Mhe. Dkt. Thomas Masanja ametoa rai kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika kulinda na kukuza haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika Aprili 2, 2025 katika Ofisi ya Mtendaji Kata ya Ilembula iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe Mkoani Njombe, Mhe. Dkt. Masanja amesisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya Serikali, taasisi binafsi na wananchi katika kukuza na kulinda haki za kiraia, kisiasa  haki za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni kama zilivyoainishwa katika Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu.

Dkt. Masanja alieleza kuwa THBUB imejipanga kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha haki za kila Mtanzania zinalindwa na kukuzwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Sheria za nchi.

"THBUB ipo kwa ajili ya kuhakikisha kuwa haki za kila mtanzania zinakuzwa, kulindwa na tumejipanga kushirikiana na wadau wote mkiwemo wananchi ili kuhakikisha kila mtu anapata haki zake bila ubaguzi wowote "amesema Dkt. Masanja
Aidha, Dkt. Masanja alihimiza wananchi kutoa taarifa juu ya vitendo vyote vya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia, matumizi mabaya ya madaraka na ubaguzi wa aina yoyote.

Aidha, Wananchi wa Kata ya Ilembula walipata fursa ya kuuliza maswali na kutoa maoni yao kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na haki za binadamu na utawala bora ambapo wengi wao walipongeza juhudi za zinazofanywa na THBUB katika kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa utawala wa sheria na uwajibikaji kwa viongozi



*Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Mhe. Dkt. Thomas Masanja akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Aprili 2, 2025 katika Ofisi ya Mtendaji Kata ya Ilembula iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Mkoani Njombe.*



*Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Mhe. Nyanda Shuli akitoa neno la ufunguzi katika mafunzo ya maadili na uwajibikaji katika utumishi wa umma yaliyotolewa kwa watumishi wa THBUB Tawi la Dar es salaam, ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya THBUB Jijini Dar es salaam, Mei 27, 2025.*

# Watumishi wa THBUB watakiwa kuzingatia maadili ya Utumishi wa Umma

Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Tawi la Dar es salaam wametakiwa kuzingatia maadili na kanuni za utumushi wa umma wakati wakitekeleza majukumu yao ili kuweza kukuza heshima ya Tume na Serikali kwa ujumla.

Wito huo umetolewa na Kamishna wa THBUB, Mhe. Nyanda Shuli wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya maadili na uwajibikaji katika utumishi wa umma yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya THBUB, Jijini Dar es salaam Mei 27, 2025

Mhe. Shuli amesema mafunzo hayo ni umuhimu kwa watumishi kwani yatasaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao na kukuza utendaji kazi unaozingatia uwajibikaji na uadilifu.

"Mafunzo haya ni muhimu kwani yatasaidia kutimiza wajibu wetu kama watumishi wa umma na kwamba kanuni za maadili zipo kutuelekeza namna nzuri ya kuenenda sisi kama watumishi wa umma hasa katika jamii zetu." amesema Mhe. Shuli

Akiwasilisha mada ya Maadili na Uwajibikaji Katika Utumishi wa Umma, Bi. Grace Matunda, Afisa Uchunguzi Mkuu kutoka Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Kanda Maalum ya Dar es Salaam ameeleza kuwa watumishi wa umma wanapaswa kuzingatia misingi ya maadili, sheria na kanuni katika utoaji huduma kwa wananchi. Aidha, Bi. Grace amesisitiza kuwa watumishi wa umma wanao wajibu wa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu, uaminifu na uwazi ili kukuza dhana ya utawala bora nchini.

Mafunzo hayo ya siku moja yamefanyika kwa lengo la kukuza uadilifu na uwajibikaji kwa watumishi wa umma ili kukuza ubora wa huduma na viwango vya utendaji kazi unaozingatia haki za binadamu na utawala bora.

# VIJANA WAASWA KULINDA AMANI NCHINI

Katika kudumisha na kuimarisha amani ya nchi, vijana waaswa kuwa mstari wa mbele kuilinda.

Wito huu umetolewa na Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Mhe. Amina Talib Ali wakati wa kuadhimisha Siku ya Sheria iliyoandaliwa na Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dodoma iliyofanyika Aprili 25, 2025 katika Ukumbi wa CIVE Auditorium ulipo chuoni hapo. Kauli mbiu ya Kongamano hilo ilikuwa ni "Nafasi ya Kliniki za Sheria za Vyuo Vikuu katika kuhakikisha Uchaguzi Huru, Haki na Uwazi Tanzania"

Mhe. Amina amesema kuwa amani ni muhimu sana nchini kabla na baada ya uchaguzi hivyo, jamii ihakikishe kuwa maandalizi yote ya uchaguzi yanafanyika kwa amani bila kuleta machafuko.
"Ni wajibu kila mwananchi kuhakikisha kwamba tunakwenda kwenye uchaguzi kukiwa na amani'

Pia, Mhe. Amina amesema kuwa miongoni mwa haki zilizoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 ni uhuru wa kutoa maoni na haki ya kushiriki katika shughuli za uongozi ikiwemo kuchagua au kuchaguliwa.

"Hivyo kila mmoja wetu ajue kwamba anayo haki ya kushiriki katika masuala ya uchaguzi lakini hakikisha unafuata Sheria, miongozo na taratibu zilizowekwa' amesema Mhe. Amina.

Kwa hatua nyingine Mhe. Amina ameupongeza Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa kuchagua mada hiyo ambayo imeenda sambamba ikiwa tunaelekea katika uchaguzi mkuu mwaka huu



*Kamishna Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Mhe.Amina Talib Ali akizungumza na Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakati wa kuadhimisha siku ya Sheria Aprili,2025 katika Ukumbi wa CIVE uliopo chuoni hapo*




*Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, (THBUB) Bw. Patience Ntwina akizungumza na watumishi wa ofisi hiyo ( hawapo pichani), wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya Maadili na Uwajibikaji katika Utumishi wa Umma, Lishe, Afya akili na Magonjwa sugu yasiyoambukiza mahali pa kazi yaliyo fanyika katika Ukumbi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Dodoma Aprili 16, 2025*

# THBUB na DIHR zawajengea uwezo watumishi kuhusu haki za wavuvi wadogo

Watumishi wa THBUB wamejengewa uwezo kuhusu haki za wavuvi wadogo wadogo katika kuwaongezea watumishi uelewa wa masuala yanayoathiri zamii za wavuvi katika matumizi na usimamizi wa rasilimali za bahari.

Mafunzo hayo ya siku moja yaliyofunguliwa na Katibu Mtendaji wa THBUB, Bw. Patience Ntwina, yaliyofanyika katika Ukumbi wa mikutano wa Hotel ya Four Points, Jijini Dar es salaam Aprili 9, 2025.

Akibainisha ushirikiano uliopo kati ya THBUB na wadau katika kukuza na kuhifadhi haki za binadamu nchini, Bw. Ntwina amesema kuwa mafunzo yaliyotolewa yametokana na ushirikiano uliopo baina ya THBUB na Taasisi ya Kitaifa ya Haki za Binadamu Denmark (DIHR) ambapo kwa pamoja wamekuwa wakitekeleza miradi mbalimbali hususani katika eneo la haki za binadamu na biashara " amesema Bw. Ntwina

Aidha, Bw. Ntwina ametoa wito kwa washiriki hao kushiriki kikamilifu mafunzo hayo ili kuweza kutimiza jukumu la THBUB la kukuza na kulinda haki za binadamu na kuweza kutoa maoni ambayo yatasaidia Serikali pamoja na wadau kubuni jitihada za kuimarisha rasilimali za bahari.

Akiongea kwa niaba ya washiriki, Mfawidhi wa Ofisi ya THBUB Tawi la Mtwara Bw. Juma Mleli, amesema kuwa mafunzo hayo yatawaongezea uelewa na hivyo kuyatumia mafunzo hayo katika kuwaelimisha wavuvi wadogo wadogo pamoja na wafanyabiashara wa mazao ya bahari ili waweze kujua haki zao wakati wakifanya shughuli zao katika fukwe za bahari.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na THBUB kwa kushirikiana na Taasisi ya Kitaifa ya Haki za Binadamu Nchini Denmark (Danish Institute of Human Rights- DIHR) ambapo washiriki walikuwa ni watumishi kutoka THBUB, wawakilishi wa wavuvi wadogo kutoka Tanga, Kilwa-Lindi, Dar es Salaam, Mwakilishi wa Wizara ya Uvuvi na Mifugo pamoja na wawakilishi kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Bindamu na Kutoka DIHR.

# THBUB YATOA ELIMU YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA KWA MAAFISA WA JESHI LA POLISI

Maafisa kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Tawi la Dar es salaam, wametoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora kwa Askari 955 wa Jeshi la Polisi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Mafunzo hayo yaliyokuwa na lengo la kukuza na kuimarisha haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa Jeshi la Polisi Tanzania yalifanyika katika Chuo cha Dar es salaam Police Academy (DPA) Aprili 10,2025

Akitoa mafunzo hayo, Afisa Uchunguzi Mkuu kutoka THBUB, Bw. Francis Luziga alisema kuwa, Serikali kupitia wizara, idara na taasisi mbalimbali likiwemo Jeshi la Polisi imeendelea kuweka misingi imara ya kuhakikisha haki za binadamu zinakuzwa na kulindwa.

Naye, Bw. Brighton Mwiga, Afisa Uchunguzi Mkuu aliwasisitiza maafisa hao kuzingatia misingi ya utawala bora katika vituo vyao vipya vya kazi ili kuboresha utendaji kazi wao katika dhana nzima na ulinzi wa raia na mali zao.

Mafunzo hayo yamehusisha Maafisa wa Jeshi la Polisi (ASP) na Wakaguzi (Assistant Inspectors) wa Jeshi la Polisi Tanzania Bara na Zanzibar.



*Afisa Uchunguzi Mkuu kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala(THBUB) Bw.Francis Luziga akitoa elimu ya haki za binadamu kwa Askari wa Jeshi la Polisi kutoka Tanzania bara na Zanzibar katika Ukumbi wa Chuo cha Polisi Dar es Salaam Aprili 10,2025.*




*Makamu Mwenyekiti Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mhe.Mohamed Khamis Hamad akiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wa THBUB Makao Makuu wakati alipotembelea Banda la THBUB katika Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma Juni 17, 2025*

# THBUB yahimiza wananchi kupata ushauri wa kitaalamu ili kujua sheria za ardhi.

Wananchi wa Mkoa wa Dar es salaam wahimizwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu pamoja na kuzijua sheria na taratibu za utwaaji wa ardhi kabla na baada ya kufanya manunuzi ya ardhi ili kujiridhisha kuhusu uhalali wa eneo husika.

Wito huo umetolewa Juni 19, 2025 na Afisa Uchunguzi Mkuu kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Bi. Juliana Laurent wakati akiwahudumia wananchi mbalimbali waliotembelea Banda la THBUB katika Kampeni ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia viwanja vya Maturubai vilivyopo Mbagala Manispaa ya Temeke, Jijini Dar es salaam. Bi. Juliana ametoa wito huo mara baada ya kupokea idadi kubwa ya malalamiko yanayohusu migogoro ya ardhi, hali inayoonesha kwamba kuna changamoto ya uelewa kuhusu taratibu za utwaaji wa ardhi.

”Migogoro mingi ya ardhi inatokana na watu kununua ardhi kiholela bila kufuata sheria, pia ni muhimu kufuata hatua zote na kupata ushauri kutoka kwa wataalamu wa ardhi na wanasheria.” Amesema Bi. Juliana

Aidha, amewataka wananchi kufanya uhakiki katika ofisi za Serikali za Mitaa, Halmashauri za Miji na Wilaya au Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi ili kubaiani kama ardhi hiyo imepimwa, ina hati na haina mgogoro wowote.

Ushiriki wa THBUB katika kampeni ya msaada wa kisheria wa Mama Samia umekuwa na mafanikio makubwa ambapo jumla ya wananchi 196 walifika katika banda la THBUB wakiwa na malalamiko mbalimbali ambayo yalipokelewa na kupatiwa ufumbuzi.

Mbali na migogoro ya ardhi, malalamiko mengine yaliyopokelewa kwa wingi yanahusiana na mirathi, migogoro ya ndoa, malezi ya watoto pamoja na masuala ya ajira.




***Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Mhe. Khatib Mwinyichande akikabidhiwa Mti wa kupanda na Balozi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma Bw Julian Bruno katika Bustani ya Miti iliyoko Nkuhungu Jijini Dodoma kwa lengo la kuimalisha haki ya Kuishi Mazingira safi na salama Juni 20, 2025***

# THBUB YAIMARISHA HAKI YA KUISHI KWA KUPANDA MITI

Viongozi na Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) wameshiriki katika zoezi maalum la upandaji miti lililofanyika katika bustani ya Tume hiyo iliyopo Nkuhungu, jijini Dodoma kwa lengo la kuimarisha haki ya kuishi, mazingira safi na salama Juni 20,2025.

Akizungumza wakati wa tukio hilo Makamu Mwenyekiti THBUB Kamishna Mhe.Mohamed Khamis Khamad amesema kuwa Tume inafahamu changamoto mbali mbali zinazohusu mazingira hivyo zoezi hilo ni katika kuendeleza juhudi za Serikali katika kutatua changamoto hizo.

“Upandaji miti si tu zoezi la kimazingira, bali ni hatua ya kuimarisha haki ya kila Mtanzania kuishi katika mazingira salama, jambo ambalo lina uhusiano wa moja kwa moja na afya, usalama na ustawi wa jamii,” amesema Mhe.Hamad.
Kwa upande wake Mwenyekiti wa Mtaa wa Salama Kata ya Nkuhungu

Bw. Abbas Mwijuki ameshukuru Tume kwa kusaidia kuhifadhi na kuboresha eneo hilo kwani miti hiyo imesaidia kupunguza upepo na kupata eneo la kivuli kwa ajili ya kivuli wakati wa jua

Bw. Mwijuki amewataka wananchi kuhakikisha wanatunza vyema miti hiyo na kuhakikisha kila mwananchi anapanda miti katika mazingira yake ili kuendelea kuboresha mazingira yanayowazunguka.

Naye Balozi wa Mazingira mkoa wa Dodoma Bw. Julian Bruno amepongeza THBUB na ameeleza kuwa Tume imekuwa ikitoa mchango mkubwa katika kuhakikisha mazingira yanatunzwa na kuhakikisha uhai wa binadamu unaendelea kuwepo.




*Naibu Katibu Mtendaji Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora,Bw. Juma Msafiri Karibona (Katikati) akiwa na maofisa wa THBUB ofisi wakati wa ufunguzi wa Kampeni wa Msaada wa Kisheria wa Mama Samia katika Viwanja vya Mwanamashungi, Wilaya ya Chakechake Mkoa wa kusini Pemba Mei 05, 2025.*

## "TUNAJIFUNZA"




*Mfawidhi Tume ya Haki za binaadamu na Utawala Bora, Saada Ahmeid Masoud akizungumza na wananchi waliofika katika Banda la THBUB wakati wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia, viwanja vya Donda, Mtende Mkoa wa Kusini Unguja, Mei 12, 2025.*

# MAWASILIANO

**Mtaa wa Nyerere,** Plot Na. 339/Kilimani
S.L.P 1049 DODOMA, Tanzania
Simu: +255 738 279744
Barua Pepe:
**www.chragg.go.tz**